

BALOZI WA TANZANIA BAHRAIN MWENYE MAKAZI YAKE ABU DHABI AWASILISHA HATI ZA UTAMBULISHO KWA MFALME WA BAHRAIN

Tarehe 22 Aprili, 2025 Mhe. Lut. Jen (Mst) Yacoub Hassan Mohamed, Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Bahrain mwenye makazi yake Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu amewasilisha hati za Utambulisho kwa Mfalme wa Bahrain katika Ikulu ya Mfalme huyo mjini Manama, Bahrain.

Tanzania na Bahrain zilianzisha muhusiano ya kidiplomasia toka mwaka 1978 mahusiano hayo yamekuwa yakikuwa hususan kiuchumi. Hadi sasa Tanzania inauza zaidi nchini Bahrain bidhaaa mbalimbali ikiwemo nyama ya kondoo au mbuzi; minofu ya samaki mbich au waliogandishwa; mbogamboga, karafuu; mananasi, parachichi, mapera, maembe, maua, madini n.k.

Kwa upande mwingine, Tanzania inaweza kunufaika zaidi na Bahrain katika sekta za mafuta ya Petroli na Gesi, Waya za Alumini, Mbolea ya Nitrojeni ya Kemikali, Mashine na Vifaa vya Umeme, n.k.

Hivyo, kuwasilisha Hati za Utambulisho kwa Mheshimiwa Balozi kutafungua fursa zaidi za ushirikiano kiuchumi na kuongeza zaidi biashara na uwekezaji kati ya nchi hizi mbili zaidi ya sekta tajwa.